Toleo 15

# Ukweli wa Injili

*SHAURI LA KIBIBLIA NA HIMIZO KWA WATENDAKAZI ULIMWENGUNI KOTE*


## "ENENDENI NANYI MKATENDE VIVYO HIVYO."

*(Ifuatayo ni hadithi ya mifano ambayo Alinena Yesu katika kitabu cha Luka 10: 25-37)*

Kwa kupigwa na kujeruhiwa vibaya, Myahudi aliyetembea kwenye njia kuu ya vumbi kuelekea Yerusalemu karibu afe. Alinyang'anywa mali yake na mavazi yake na kuachwa nzi zikimlamba na jua kumchoma mwili uliokuwa uchi, hangeweza kujisaidia kwa maana mwili wake uliendelea kuwa dhaifu sana.

Mwangaza wa tumaini ulionekana kuingia kwake kupitia hali yake ya machungu na majonzi alipotazama na kuona mtu akimkaribia. Msaada ulikuwa ukimjia. Kuhani aliyekuwa mtumishi wa Bwana alipita pale na kuona hitaji la mtu Yule, alipita na kutembea upande mwingine wa barabara, asije akacheleweshwa katika safari yake na kazi hiyo isiyo ya maana. Alipita na kuenda zake asijali mtu yule mahututi.

Punde baada ya hapo mlawi naye akafika na kupita. Alisimama kidogo akamtazama mtu yule mahututi kwa umbali na mlawi akavuka upande mwingine na kuendelea na safari.



Uzima ulikua ukiendelea kumtoka wakati vidonda viliendelea kuvuja damu. Alikuwa amechoka akiwa katika uchungu na bila tumaini. Kama watu wa dini walipita bila kusaidia mtu yule alikaribisha giza la afya lililokuwa likimzunguka ili aliwaze hali yake.

Ghafla mtu yule alihisi mkono wa mtu ukimgusa kwa upole katika vidonda vyake. Aliinua kichwa chake kwa mbali akasikia sauti, "Rafiki, inuka unywe" maji baridi ndani ya kinywa chake.

Alipozidi kutambua mazingira yake aligundua alikuwa mtu msamaria aliyemhudumia.Wasamaria walikuwa watu waliodharauliwa na kutengwa na Wayahudi na sasa huyu Msamaria alikuwa akiyaokoa maisha yake. Msamaria alimwinua Myahudi yule na kumweka juu ya punda wake na kumpeleka katika Nyumba ya wageni na kumlipa mlinzi wa nyumba ya wageni kumhudumia yule Myahudi mgonjwa. "Nitarudi kulipa chochote ulichogharimiwa Zaidi."

Yesu alitoa mfano huu ili ajibu swali lililoulizwa na wakili (mwanasheria) Yesu na wakili yule walikubaliana kuwa uzima wa milele unapeanwa kwa wale wanaompenda Mungu kwa moyo wao wote na wanaowapenda jirani zao kama wanavyojipenda wenyewe.

*(Endelea ukurasa wa 2)*


Tahariri 3

Uchambuzi wa Biblia: Matendo ya Msaada 4

Jarida la Ushirika: Matendo ya Msaada 5-6

Maswali na Majibu 7

Je, Ulijua? Tupa Chakula Chako Usoni Pa Maji 8

# MAMBO AMBAYO
# BIBLIA
## Inafundisha Kuhusu...

**Neno la Mungu**
2 Tim. 3:6, 2 Pet. 1:20-21, Mt. 24:35
**Uhusiano wa Upendo**
Mt. 22:37-40, Yn. 14:21-23, 1 Yoh. 4:7-21
**Toba**
Mdo. 3:19, 17:30, 2 Kor. 7:10
**Uzao Mpya**
Yn. 3:3-7, 2 Kor. 5:17, Rum. 6:1-4, Efe. 2:1, 5-6
**Uhuru Kutokana na Dhambi**
1 Yoh. 5:18, Mt. 1:21, Yn. 8:11
**Ujazo wa Roho Mtakatifu**
Mdo. 19:2, 15:8-9, 1:8
**Utakatifu**
Lk. 1:73-75, Ebr. 12:14, 1 Pet. 1:15-16, Tit. 2:11-12, Rum. 6:22
**Ufalme wa Mungu**
Lk. 17:20-21, Rum. 14:17, Yn. 18:36
**Kanisa**
Mdo. 2:47, Efe. 4:4-6, 1 Kor. 12:12-13, Kol. 1:18
**Umoja**
Yn. 17:20-23, Gal. 3:28, Ufu. 18:2-4
**Kanuni za Kanisa**
Mt. 28:19-20, 26:26-30, 1 Kor. 11:23-27, Yn. 13:14-17
**Uponyaji wa Kiungu**
Lk. 4:18, Isa. 53:4-5, Yak. 5:13-16
**Utakatifu wa Ndoa**
Mt. 19:5-6, Lk. 16:18, Rum. 7:2-3, 1 Kor. 7:10-11
**Urembo wa Nje**
1 Tim. 2:9-10, 1 Kor. 11:14-15, Kum. 22:5
**Mwisho wa Nyakati**
2 Pet. 3:7-12, Yn 5:28-29, 2 Kor. 5:10, Mt. 25:31-46
**Kupenda Amani**
Lk. 6:27-29, 18:20
**Ibada**
Yn. 4:23-24, Efe. 5:19, 2 Kor. 3:17
**Wajibu Mkuu**
Mk. 16:15

*(Endelea kutoka ukurasa 1)*

Lakini, “Ni nani aliye jirani yangu?” Wakili akauliza. Yesu akamwambia mfano huu wa msamaria mwema.

Jirani wa kweli hakuwa mtu wa rangi moja naye au kabila. Hakuwa yule aliyemwaminifu wa kuabudu hekaluni. Jirani wa kweli alikuwa mgeni, yule aliyejitolea kusaidia wakati wa hitaji. Upendo kama huo ndio unaofungua mbingu.

Uzima wa milele ingawa ni kipawa cha Mungu hupeanwa kwa wale wampendao Mungu na wanadamu wenzao. Upendo haupo katika maneno bali katika matendo. Kuna wengi katika dunia yetu, iwe ng’ambo ya bahari au katika barabara wanaoumia na wahitaji msaada, Wakristo huonyesha upendo wa Mungu kwa kuwasaidia wasiojiweza, huu ndio msingi wa maisha ya Kikristo. Watu wengi huzingatia sana haki yao na utauwa lakini hudunisha majukumu ya kutoa mahitaji yanayoonekana, hisia nay a kiroho kwa wanadamu.

Msamaria aliyehudumia kimatendo yule aliyejeruhiwa, uikuwa mfano wa Yesukwa wanaowapenda jirani wao kama wanavyojipenda. Basi Kristo akamwambia wakili jinsi asemavyo leo, “Enendeni nanyi mkatende vivyo hivyo.”

—mws

### UKWELI WA INJILI

Gazeti la ‘*Ukweli wa Injili’* huchapishwa kwa jina la Bwana kwa matumizi ya watu wa mataifa yote kwa kusudi la kuimarisha na kuwahimiza watu wote katika ukweli wa neno la Mungu. Gazeti hili hufundisha na kueneza ukweli wa Biblia ambao umethibitishwa tangu nyakati za Yesu Kristo na mitume.

Neno la Mungu ndio mwongozo halisi na wa kipekee wa imani. Linafundisha wokovu na ukombozi kutokana na dhambi unaoletwa na utakaso wa Yesu Kristo; ambao hufuatiwa na ujazo wa Roho Mtakatifu anayemwongoza mhudumu, kumwonyesha njia, na kumpatia nguvu; pia unamletea mtu utakatifu halisi katika kila fani ya maisha yake; na pia kuleta umoja na utangamano wa watu wa Mungu. Huduma inayokubalika na Mungu inatokana na mtu kuwa na uhusiano wa kibinafsi na wa upendo ambao msingi wake ni ukweli.

Waandishi: Michael na René Smith

### UAGIJAJI

*Ukweli wa Injili* ni gazeti la kieletroniki linalochapishwa kila robo ya mwaka jinsi mungu anavyotuongoza. Tutembelee katika tovuti yetu ya www.thegospeltruth.org ili uagize jalida hili kupitia kwa orodha yetu ya anwani pepe na upokee toleo lako la wakati huu. Hebu jisikie huru kututumia orodha ya majina na anwani pepe za watu wengine ambao wangependa kupokea toleo hili kutoka kwa mwandishi wa jalida la Ukweli wa Injili.

### ANWANI

Gazeti a *Ukweli wa injili* linachapishwa katika mataifa mbalimbali ili kusambazwa katika maeneo hayo. Kazi hii na zingine za kimishenari ambazo sisi hufanya huwezekana kupitia kwa matoleo ya kujitolea yanayotolewa kwa jina la Kanisa la Mungu.

Ukweli wa Injili, 605 Bishops Ct., Nixa, MO 65714 USA
editor@thegospeltruth.org

# *Tahariri*



*"Amin nawaambia, kadiri mlivyomtendea mojawapo wa hao ndugu zangu walio wadogo, mlinitendea mimi."* —Matthew 25:40

Yesu aligawanya kondoo na mbuzi, waliookoka na wasiookoka kutokana na kuzingatia matendo yao mema, bila kubatilisha hitaji la wokovu. Yesu alionyesha umuhimu wa matendo mema, kazi ya msaada. Jinsi gani? Kama watu wa Mungu, Je, tunawezaje kupuuzia nguvu ya matendo mema? Nguvu ya Imani, nguvu ya utauwa na mavazi mema ni nini kama hakuna upendo uletao kujitolea kwa wasiojiweza na wale waliolemewa.

Tunavyowahudumia wenzetu, twahudumia Kristo mwenyewe – kikombe cha maji baridi, kuzuru wagonjwa, wimbo kwa waliofungwa, neno la upole kwa wazee, blanketi kwa walio na baridi, mkate kwa walio na njaa, kufungwa kidonda kwa wanaovuja damu ni Baraka na tunuku jinsi gani kutoa kwa aliye na hitaji.

Baadhi ya furaha nyingi maishani mwangu imetokana na kujitolea kwangu. Nimejifunza pia heri kukosa ili mtumishi wa Mungu apate riziki ya kujaza hitaji lake. Jinsi hii ndivyo Mungu alivyotengeneza mpango wa wokovu.

Ninapenda ukweli na mafundisho ya neno la Mungu. Tumaini langu ni kushikilia bendera ya Yesu na utakatifu unaoonekana wa maisha ya matendo. Ninaeneza katika toleo hili la ukweli wa injili, ukweli halisi wa mafundisho ya matendo ya msaada. Kama watoto wa Mungu, maisha yetu yanafaa kusisimuliwa na upendo na matendo ya asili ya msaada kwa wenzetu. Hili si jambo au kitu cha hiari cha kufanya unapopenda au kuacha bali ni amri ya Mungu na ndio moyo wa Kristo.

Wengine husema msaada, wema si kazi ya Mungu bali huduma kubwa ni kushiriki injili na dunia, sehemu ya kazi ya Mungu ni kuhudumia mahitaji ya kiasili yanayowakumba watu. Mengi yamenenwa kwa wingi katika maandiko na ombi langu ni kwamba macho yetu yafunguke katika sehemu hii. Ni mwito wetu sote.

Wakati mwingine tunashangazwa na kinachosisimua watu wanapokuja kusikiliza injili na pia kupokea msaada wa kibinadamu, kwa nini wako hapa? Mwisho wa siku ninahimizika kuwa Yesu aliwaambia makundi "Mwanitafuta si kwa kuwa mliona miujiza bali ni kwa sababu mlikula mikate na mkashiba."

Yesu bado aliwalisha makundi kwa sababu ya huruma, na ndivyo ilivyo kwetu leo.Katika kuwahudumia wengine, tunashiriki upendo wa Yesu Kristo mwenyewe.

Tunaweza kuwa na maono ya Msamaria ili kuona mahitaji ya watu katika dunia yetu na tusiweze kuwasaidia kwa kujitolea.

Michael W. Smith

January 2016



mengi kwa

MTANDAO

*Tutembelee kwa*

*www.thegospeltruth.org*

*ili uagize na kusoma*

*jarida letu.*

# MWONGOZO WA UCHAMBUZI WA BIBLIA

## SOMO: MATENDO YA MSAADA



**Ombi (Sala) juu ya Matendo ya msaada**

*Ikiwa nimewanyima maskini haja zao, au kama nimeyatia kiwi macho ya mwanamke mjane;*

*Au kama nimekula tonge langu peke yangu, mayatima wasipate kulila (La, tangu ujana wangu alikuwa pamoja nami kama kwa baba);*

*Nami nimekuwa kiongozi cha mjane tangu tumbo la mamangu; Ikiwa nimemwona mtu kuangamia kwa kukosa nguo, au wahitaji kukosa mavazi;*

*Ikiwa viuno vwake havikunibarikia au kama hakupata moto kwa manyoya ya kondoo zangu;*

*Ikiwa nimewainulia mayatima mkono nilipoona msaada wangu mlangoni, basi bega langu lianguke kutoka mahali pake, na mkono wangu uvunjike mfupani mwake.*

*Ayubu 31:16-22*

**Maandiko:** *Ikiwa ndugu mwana mume au ndugu mwanamke yu uchi na kupungukiwa na riziki na mtu wa kwenu akamwambia, Enendeni kwenu na amani na mkaote moto na kushiba lakini asiwape mahitaji ya mwili yafaa nini? Vivyo hiyo na imani isipokuwa ina mateno imekufa nafsini mwake.*
*—Yakobo 2:15-17*

**Hitimisho:** Matendo ya huruma na msaada ni somo la msingi kwa maisha ya Mkristo. Upendo wa Mungu wa kweli na Imani ya Kidini inaonekana katika kujitolea katika huduma kwa walio na mahitaji na wasiojiweza.

### I. Upendo unadhihirishwa katika matendo ya huruma

A. Mathayo 22:37-40 Msingi wa Upendo.
B. Luka 10:25-37 Msamaria Mwema.
C. I Yohana 3:17-18 Upendo Katika Matendo.

### II. Mifano katika agano jipya.

A. Matendo 10:38 Yesu Alitenda Mema.
B. Mathayo 15:32-39 Umati Ukalishwa.
C. Warumi 15:26-27 Wateule Wafanya Mchango kwa Maskini.
D. Matendo 9:36 Dorcas–Mwingi wa Matendo Mema.
E. Agano la Kale: Ayubu 31:16-22

### III. Mwanadamu aliokolewa amtukuze Mungu katika matendo

A. Mathayo 5:14-16 Matendo Mema ni kama Nuru kwa Ulimwengu.
B. Waefeso 2:8-10 Kuumbwa kwa ajili ya Matendo Mema.
C. Tito 2:14 Uchu wa Matendo Mema.

### IV. Matendo mema/ msaada imeamiwa

A. Isaya 58:7 Wema Umeamriwa.
B. I Timotheo 6:17-18 Tayari Kugawa.
C. Tito 2:7 Onyesha Msururu wa Matendo Mema.
D. Tito 3:8 Endeleza Matendo Mema.
E. Wahebrania 10:24 Sisimuka kwa Matendo Mema.
F. Wagalatia 2:9-10 Kumbuka maskini.
G. Waefeso 4:28 Kutoa Kumsaidia mtu Aliye Maskini.
H. Wagalatia 6:10 Wema kwa Kila Mtu.

### V. Matendo ya msaada yanadhihirisha

A. Yakobo 1:27 Dini ya Kweli.
B. Yakobo 2:14-18 Imani ya Kweli.

### VI. Baraka katika kutoa

A. Matendo 20:35 Baraka Nyingi kwa Wanaotoa.
B. Luka 14:13-14 Malipo katika Umilele (Mbinguni).

### VII. Hukumu ya mwisho

A. Ufunuo 20:12-13 Kulingana na Matendo.
B. Mathayo 25:31-46 Kulingana na Matendo Mema.

**Hitimisho:**

*Lakini mtu akiwa na riziki ya dunia; kisha akamwona ndugu yake ni mhitaji, akamzuilia huruma zake, Je, upendo wa mungu wakaaje ndani yake huyo? Watoto wadogo, tusipende kwa neon au ulimi, bali kwa tendo na kweli.*

—I Yohana 3:17-18

# MATENDO YA MSAADA

Nakala ya kuandamana na Mafunzo ya Biblia

### Msingi wa upendo

Yesu alisema kwamba amri kuu ni kumpenda Mungu na ya pili ni kuwapenda wenzetu kama tunavyojipenda (Mathayo.22:37-40). Upendo ni zaidi ya neno tu la maarifa, ni uamuzi na chaguo la moyoni, ni jukumu, na kusudi ambalo linachochea tendo. Upendo kwa mungu unadhihirika katika kutii neno lake. Upendo kwa wenzetu unadhihirika katika matendo ya huruma na msaada. Bila upendo kama huo, watu hawatampendeza Mungu wala kutekeleza kusudi la mungu katika maisha yao. Maisha ya muumini yanafaa kujaa na matendo ya msaada.

### Msamaria mwema

Msamaria mwama (Luka 10:25-37) ni mfano ambao Yesu alitupatia tufuate tunapowatumikia watu kwa mahitaji. Mkristo akiona mtu ana hitaji na asisukumwe na huruma, upendo wa mungu wakaaje ndani yake huyo? "Watoto wadogo, tusipende kwa neno, wala kwa ulimi bali kwa tendo na kweli" (Waraka wa kwanza wa Yohana 3:17-18). Maisha ya mkristo yanafaa kwenda zaidi ya kuhudhuria kanisa, kuomba na kuamini mafundisho ya ukweli. Yanafaa kuhusika na kujitolea na juhudi kwa walio na mahitaji.




### Yesu alitoa mfano mwema wa matendo

Yesu alienenda kotekote akitenda mema kwa kipindi cha maisha yake mafupi duniani (Matendo 10:38). Hakufundisha tu na kuhubiri Mungu bali aliwaponya wagonjwa, akatembelea wenye dhambi na kulisha wenye njaa (Mathayo 15:32-39). Alikuwa mtu mwenye huruma na alihudumia walio maskini katika mahitaji yao ya kimwili. Dorcasi anatajwa katika Matendo 9:36 kama mwanamke "aliyekuwa amejaa matendo mema na sadaka alizozitoa." Waumini katika kanisa la kwanza walitoa mara kwa mara kwa walio maskini (Warumi 15:26-27) na kuhudumia walio na mahitaji.  Wanahistoria wa kanisa la kwanza walikiri kuwa, misaada isiyo ya kawaida ndiyo iliyokuwa  msingi katika uenezaji wa haraka na upanuzi wa injili na ukristo. Hili ndilo ripoti linalohitajika kwa waumini wa leo katika jamii ya kijijini na kimataifa.Watu wanafaa kujulikana kwa tendo la upendo na msaada.

### Matendo mema humtukuza Baba yetu

"Vivyo hivyo nuru yenu na iangaze mbele ya watu, wapate kuyaona matendo yenu mema, wamtukuze baba yenu aliye mbinguni" (Mathayo 5:16). Kusudi la tendo la msaada sio la kutafuta umaarufu wala kuonekana na watu bali matendo mema yanaangaza upendo wa mungu katika dunia ya giza. Kupitia matendo mema, watu waone Baba na kuvutwa katika wokovu.

### Tumeumbwa kwa ajili ya matendo mema

Matendo ya msaada hayaokoi mtu lakini "tuliumbwa katika kristoYesu tuyatende matendo  mema ambayo tangu awali Mungu aliyatengeneza ili tuenende nayo" (Waefeso 2:8-10). Tena mojawapo ya makusudi makuu ya mtoto wa mungu ni kutembea katika matendo mema. Hili linaenda zaidi ya matendo ya kutafuta utakatifu wa kibinafsi na huhusisha kujitoa muda na fedha kwa ajili ya wegine walio na mahitaji. "Mwibaji asiibe tena; bali afadhali afanye juhudi, akitenda kazi ilio nzuri kwa mikono yake mwenyewe, apate kuwa na kitu cha kumgawia mhitaji" (Waefeso 4:28).

### Matendo mema yameamriwa

Maandiko yanafundisha kuwa walio matajiri (walio na ya kusaza) wanapaswa kuwa "matajiri wa matendo mema" na "tayari kushiriki mali yao" (I Timotheo 6:17-18). Muumini anashauriwa kuwa "kielelezo cha matendo mema" (Tito 2:7) na pia "wakumbuke kudumu katika matendo mema" (Tito 3:8). Mtoto wa mungu ni vyema kujihadhari kwa kuwa shauku na majukumu ya maisha yataanza kuondoa hali ya kufanyia wengine. Watu wengi siku hizi wana ubinafsi na hawana muda wa kutosha au fedha za kutoa kwa walio na mahitaji. Hii ni shida ya kiroho. Paulo anawatia changamoto waumini ili

*(Endelea kwa ukurasa 6)*

*"Kwa hivyo kadiri tupatavyo nafasi na tuwatendee watu wote wema..."*

*(Endelea kutoka ukurasa 5)*

"waangaliane wao kwa wao na kuhimizana katika upendo na kazi nzuri" (Wahebrania 10:24)

### Toa kadiri ya uwezo

Duniani ni mahali pana na mahitaji ni mengi. Haiwezekani mtu mmoja kutoa msaada kwa kila mhitaji aliyeko. Mungu hataki watu waishi katika hali ya kuhukumika kwa maana amebariki kila mmoja katika eneo lake au taifa lake na ufanisi. Kwa kuwa mungu amebariki, ni jukumu la mtoto wa mungu kushiriki kadri ya uwezo wa baraka aliyopewa. "Kwa hivyo kadiri tupatavyo nafasi na tuwatedee watu wote wema; na hasa jamaa ya waaminio." (Wagalatia 6:10).

### Dini iliyo safi



Watu wengine hutenganisha mwendo wao wa kiroho na hali ya msaada iliyo karibu nao. Yakobo anashauri hili kikamilifu, "Dini iliyo safi, isiyo na taka mbele za mungu baba ni hii, kwenda kuwatazama yatima na wajane katika dhiki yao na kujilinda na dunia pasipo mawaa" (Yakobo 21:27) Ajabu ni kwamba watu wengi wanatazama pande moja ya dini iliyo safi, Yaani dini safi ni kujilinda na dunia pasipo mawaa na kuishi katika utakatifu mbele za Mungu. Hili ni sawa lakini dini safi inajumuisha kazi za msaada--kutembelea mayatima na wajane na kushughulikia mahitaji yao ya mwili. "Tuwakumbuke maskini" (Wagalatia 2:9-10).

### Imani ya kweli

"Ndugu zangu yafaa nini mtu akisema ya kwamba anayo imani lakini hana matendo? Je, Ile imani yaweza kumwokoa? Ikiwa ndugu mwana mume au ndugu mwanamke yu uchi na kupungukiwa na riziki  na mtu wa kwenu akamwambia, Enendeni kwenu na amani na mkaote moto na kushiba lakini asiwape mahitaji ya mwili yafaa nini? Vivyo hiyo na imani isipokuwa ina mateno, imekufa nafsini mwake" (Yakobo 2:14-18).

Imani ya kweli na dini safi si tu haki ya mtu binafsi bali ni juu ya upendo wa mungu moyoni mwa mtu unaomsukuma kuwapenda watu wengine. Kuwa upendo na  imani ni maisha katika kuwahudumia walio na mahitaji. Kuna furaha na Baraka katika maisha ya kushiriki mali. Yesu akasema, "Ni heri kutoa kuliko kupokea" (Matendo 20:35). Watu wengi wanakosa baraka tele zinazokuja kipitia tendo la msaada. Tuzo kubwa  litakuwa uzima wa milele (Luka 14:13-14).

### Kuhukumiwa kulingana na matendo

Jesus Yesu alidhihirisha picha ya kutisha ya hukumu katika Mathayo 25:31-46.  Ya kwamba, watu hawakuhukumiwa kulingana na vipawa vyao vya kiroho, kiwango cha imani yao, au kulingana na mavazi yao au urefu wa maombi yao bali kwa matendo yao ya wema na msaada. Laiti wangelisha wenye njaa, kuvisha walio uchi, kuzuru wagonjwa na wafungwa?

Heri Maisha yetu yabadilike katika Yesu Kristo na tuhudumu kila siku kwa hiari kwa roho ya ukarimu kwa ajili ya mahitaji ya kiroho na ya kimwili ya wengine.

—mws

# MASWALI na MAJIBU

## Je, watu wanaojitoa kwa ajili ya kusaidia maskini wataenda mbinguni?

Si lazima. Kutoa na kujitoa kwa ajili ya wengine ni ishara ya wokovu ila haiwaokoi. Wote wametenda dhambi na wanapaswa kutubu na kusamehewa kupitia nguvu ya Yesu Kristo.



## Je, nimeamriwa kusaidia kila mhitaji nimwonaye?

La. Jinsi ilivyo katika kila Nyanja ya maisha ni vyema kuongozwa na Roho Mtakatifu. Ingawa ni amri kutenda wema ni lazima kuwa walinzi wazuri wa rasilmali ya Mungu ambayo ametukabidhi. Kama tutatoa kwa kila mhitaji hatutakuwa na ya kuwatosha. Endo la msaada huanza na walio wenye ushirika wa imani. Ni ushuhuda usiofaa kutoa kwa ajili ya watu wageni ilhali yule anayekaa kando nawe kwenye ibada anakaa njaa.

Tena, kila mtu ana mwito tofauti katika hali ya kutenda wema. Mtu anaweza kuwa na mwito wa kipekee kwa ajii ya kuhudumia mayatima, mwengine anaweza kuwa na mwito kwa wasio na makao mitaani na pia mwingine anaweza kuwa na mwito kwa ajili ya kulisha weye njaa katika mataifa mengine. Mahitaji haya yote ni muhimu. Kuna mahitaji mengi ya kuhusika jinsi mungu ameongoza na kuelekeza. Kumbuka mungu anatuongoza kutenda matendo mema.

## Je, Misaada yaweza Kuchochea maadili maovu na uvivu ndani ya mhitaji?

Hili ni swali nyeti na nafasi katika jarida hili hairuhusu jibu kamilifu. Msaada umeamriwa katika maandiko na asidhubutu mtu kudunisha hilo kwa ajili ya kutowajibika. Si utunzi wema kutoa fedha kwa mlevi ili anunue kileo lakini kama watoto wa mlevi wanalala na njaa kwa sababu yadhambi ya baba yao ni vyema kuwalisha hao watoto wasio na hatia. Maandiko hayakuwa yakiendeleza chama cha uhisani bali yanaamuru uhisani wa kibinafsi wa walio na upendo kusaidia walio na njaa, walio uchi na walio maskini.

Mtu akiwa mvivu na kukaa nyumbani bila nia ya kufanya kazi, kumpa mtu kama huyo chakula au fedha yaweza kuhimiza au kuchochea uvivu ndani ya mtu huyo. Kwa sehemu nyingine, mtu akikosa kazi ya kufanya ijapo anafanya kila juhudi, anastahili msaada.



Je, tunawawezesha watoto wetu tunapowalisha? Yatima hana baba wala mama wa kumlisha, kwa hivyo maandiko yanatuamuru tuhudumie mahitaji yao. Kusudi la mafundisho ya Yesu ni kusaidia wale walio na hitaji wala si wanaostahili kupewa au wale walio na uwezo wa mkurudisha au kulipia. ”Nilikuwa gerezani, hamkunizuru.” Yesu hakusema kuwa ziara ilikuwa iwe kwa mtu aliyezuiliwa kifungoni kwa madai ya uongo.

## Je, maskini wamehurumiwa wasitoe msaada?

No. La hasha. Ingawa matajiri wana uwezo mkubwa wa kutoa, Biblia inafundisha kuwa wote tutoe na kujitoa kwa ajili yaw engine. Kutoa si kwa fedha tu bali hata muda. Kama maskini hawezi kulisha anaweza kusaidia maskini kulima shamba lake kujenga nyumba au kushiriki blanketi. Kila mara kuna mtu aliye na mahitaji kuliko sisi wenyewe.

—mws

**JE, ULIJUA?**

**Misemo ya wazee/waandishi wa kanisa la kwanza kuhusu msaada na matendo mema:**

Na kama kuna kati yao aliye na hitaji au maskini, na kama hawana chakula, wanafunga kwa siku mbili au tatu ili kutoa chakula kwa wenye  hitaji la ukosefu wa chakula. —Mtetaa injili, Aristides 125 AD

Tunajua wengi kati yetu ambao wametoa (wakajiuza) katika kifungo ili wawakomboe wengine. Wengi pia wamejisalimisha katika utumwa, ili kwa gharama ambayo wamelipa watoe chakula kwa wengine. —Clement wa Rumi, 96 AD

Katika siku makapofunga hamtaonja chochote ila mkate na maji. Na vyakula ambavyo mngekula, kadirieni gharama ya chakula cha siku ile na mpeane fedha hizo kwa yatima, mjane na mhitaji. —Hermes wa Rumi (c.90-140)

**Neno Linalofaa kwa Msimu Huu**

## Tupa Chakula Chako Usoni Pa Maji


**Anwani**

The Gospel Truth
605 Bishops Ct.
Nixa, MO 65714
USA

Email:
editor@thegospeltruth.org

Utakatifu kwa Bwana


*Tupa chakula chako usoni pa maji;Maana utakiona baada ya siku nyingi  —Mhubiri 11:1*

Sulemani aliwahimiza wasomi "watupe mkate wao juu ya maji mengi." Si ovyo ovyo. Hiki kifungu kimetumika kuwahimiza watu kufanya huduma ya injili kila mahali. Ingawa hii ni kweli. Sulemai ananenena hasa kwa matendo ya msaada. Panda mbegu ya ukarimu na wema watu wote karibu nawe. Uwagawie sehemu watu saba, hata wa nane (Msitari 2).



Tupa juu ya maji mengi. Kuwa na huruma kwa watu wasiopendeka hata kama hawastahili. Jitoe kwa ajili ya yatima, mama mjane, baba mgonjwa, mzee na mwenye dhambi. Toa kama kwa Bwana na usishikilie chochote.

Na kwa wakati ufaao, Mungu atasababisha ongezeko. Hatupandi kwa ajili ya raha ya mwili bali Mungu atalipa watumishi wake waaminifu. Kutakuwa na urejesho.

—mws